# LEARNING BY EAR-"FAMILY AFFAIRS"

**Kipindi cha saba: "pamoja tunaweza"**

**Mwandishi:** Chrispin Mwakideu

**Mhariri**: Maja Dreyer

**Wahusika**: Eveline(19),msimamizi wa tume ya uchaguzi(65),Betty(12),waimbaji(12+),Roni(14),vijana (14+)

**<u>Utangulizi:</u>**

Hujambo msikilizaji na karibu katika kipindi kingine cha Noa Bongo Jenga maisha yako kuhusu maswala ya jamii – jinsi ya kuwa mshirika katika siasa. Beti alitumia ujasiri wake kumshawishi hasimu wake arudi katika uimbaji licha ya kuwa mwenye haya sana hapo awali. Walishinda rudni ya kwanza ya mashindano na sasa wameingia katika fainali. Evelyn naye amechukizwa na mahasidi wake waliomuharibia mabango ya picha yake. Leo ni leo kwa Roni na timu yake ya kandanda na Betty na kwaya yake. Je watashinda? Evelyn aliahidi kumtembelea mwenyekiti wa tume ya uchaguzi…Karibu katika kisa cha saba – ´´Umoja ni Nguvu´´

**<u>Onyesho la kwanza : takia afisi za tume ya uchaguzi..</u>**

**SFX: Mlamgo unafunguka na kufungwa**

**1.Kamishena**: Tafadhali keti. Nikusaidieje msichana mrembo?

**2.EVELINE**: Kwanza natumai sijapotea, bila shaka wewe ndiye kamishena wa uchaguzi..

**3.COMMISIONER**: Ndiyo…na wewe ni nani? Natumai wewe si muangalizi wa uchaguzi kutoka mikoani. Tumechoshwa na nyinyi. Tunaweza kuusimamia uchaguzi huu pekee yetu kwa ufanisi mkubwa..

**4.EVELINE**: Shukran.. nafurahi kusikia hayo. Mimi naitwa Eveline Mapito. Nagombea kiti cha udiwani wa Milimani. Timu yangu ya kampeni imetii sheria zote zha kampeni ya amani bila kumtisha mtu peyote …

**5.COMMISIONER**: Vyema! Nafurahi kusikia hayo. Sasa.. kuna yeyote anayekuzuia kufanya kampeni yako?

**6.EVELINE**: Siku chache zilizopita tulizunguka kubandika mabango yenye sura yangu na ujumbe kutaka nipigiwe kura. Kumbuka bwana kamishna tulilazimika kulipa pesa ili mabango hayo yabandikwe. Jana mabango yangu yote yaliharibiwa na kuchanwa. Ningependa kujua vipi tume ya uchaguzi inavyoweza kusaidia.

**7.COMISSIONER**: Nasikitika sana binti, lakini hakuna lolote ofisi yangu inaloweza kufanya kusaidia.

**8.EVELINE**:(**akishangaa**) Eti nini? Lazima uwe unanitania…

**9.COMMISIONER**: Unaniona nikitabasamu au kuwa na kigugumizi? Sikiliza… hiyo ni kazi ya askari polisi.. lakini kama una ushahidi kwamba mgombea fulani alifanya hivyo, uwasilishe halafu tutachukua hatua ya kumuadhibu.

**10.EVELINE**: Kwa hivyo ni basi? Hakuna hata bango moja langu mabarabani na hakuna linaloweza kufanywa na ofisi ya tume ya uchaguzi.. Vipi kuhusu gharama za kuyachapisha mabango hayo?

**11.COMMISIONER**: **(akikasirika)** Nimekuwa nikifanya kazi kwa miaka thelathini na sijawahi kuona tume ikilipia mabango yaliyoharibiwa na wapinzani. Kazi yetu ni kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa uhuru na haki…

**12.EVELINE**: (**nguvu**) Uchaguzi unawezaje kuwa huru na wa haki wakati mabango yangu yamechanwa? Tafadhali nifafanulie maana ya uchaguzi huru na wa haki…

**13.COMMISIONER**: (**hamaki ikianza kumpanda**) Wewe unadhani ni nani, heee? Unakuja hapa kunisomea jinsi ninavyotakiwa kuifanya kazi yangu? Wewe si wa kwanza wala wa mwisho kugombea kiti cha udiwani! Huna hana heshima?

**14.EVELINE**: Nakuomba radhi.. kamwe sikunuia kukukasirisha.. wewe ni mmoja wa mifano bora kwangu… lakini nikitaraji labda kuna kitu kinaweza kufanywa ili udhalimu huu usiwepo…kama unavyoona mimi bado ni msichana mdogo..

**15.COMMISIONER**: K.S.Z.A

**16.EVELINE**:(**arudia**) K.S.Z.A? Hiyo ina maana gani nini?

**17.COMMISIONER**: Ni ufupisho wa…..Karibu Siasa Za Afrika.

**18.EVELINE**
Inasikitisha kuwa hadi sasa bado tunachaguwa mfumo wa siasa za chuki, kugawanyana, ukabila na kadhalika. Kwa nini tusiwaige wenzetu wa nchi za magharibi wanaofanya uchaguzi wao kwa amani na utulivu…

**19.COMMISIONER**: **(akipuuza)** Napendekeza upande ndege inayoondoka, meli au basi uondoke mahali hapa. Nina kazi nyingi za kufanya..

**20.EVELINE**: **(akisimama kutoka kitini)** Asante kwa wakati wako.. hata hivyo, wakati utafika..na lazima ufike.. ambapo tutakuwa na siasa za kutuunganisha na wala sio za kututenganisha.

**SFX: MLANGO WAFUNGULIWA NA KUFUNGWA**

**<u>ONYESHO LAPILI: KATIKA UWANJA WA MPIRA</u>**

**1.Kundi**: **(wakishangilia)** Milimani! Milimani!

**2.RONI**: Jamaa, leo ni leo msema kesho ni muongo..ni siku ya kufa kupona. Tumekuwa tukiifanyia mazoezi siku hii kwa majuma kadhaa. Tuchezeni kama timu moja .. nakumbuka kocha aliwahi kuniambia huu ni mchezo wa kandanda na wala si tenisi

**SFX: WAKIHEMA**

**3.RONI:** Hip Hip!

**4.VIJANA:** Hureeeee!

**SFX: Kipenga chalia**

**5.MSIMULIZI**: Na mchuano ukaanza huku Roni akibeba dhamana ya matarajio ya shule yake, familia na juu ya yote yeye mwenyewe. Wakati huo huo, katika ukumbi wa muziki…….

**<u>Scene three: At the Music Hall/ Football Match</u>**

**1.kundi**: **(kelele za kushangiliwa)**

**MSIMULIZI** : Wakiwa na hatua chache kulimudu jukwaa. Ilipofika wakati wa mapumziko tayari kikosi cha Roni kimezabwa bao moja kwa nunge…

**3.RONI**: (**akihema sana**). Yuko wapi kocha…ni muhimu awe hapa…tunamhitaji.

**4.Kijana**: **(pia akihema sana)** Roni, mkufunzi alikuamini utuongoze na unatuuliza tufanye nini..…

**5.RONI**: Ah, sawa, tuendelee kucheza kama timu moja na tuzidi kuwashinikiza.. tuwe waangalifu tusiwape tena nafasi ya kutufunga bao jengine.. tusivunjwe moyo na bao lao.. kutangulia sio kufika sawa? ……..( jibu) ….. Hip! …….Hip!.....

**6.vijana**: Sawa

**SFX:Kipenga kinalia**

**Msimulizi**: Kipindi cha pili na cha lala salama kimeanza. Na katika ukumbi wa muziki matokeo yanatangazwa ….

**Mkuu wa sakafu**: Mshindi wetu katika tamasha hili la muziki katika kitengo cha shule za msingi ni Milimani ikiongozwa na Beti Mapito!!!!

**9.Wasichana**: Hoyeeee!!!!! **(wanaanza kuimba na kushangilia)**

**10.NARRATOR: MSIMULIZI:** Huku Betty na kwaya yake wakiimba na kushangilia ushindi wao, wanashikana mikono katika duara na kusahau uhasama katikati yao. Ndoto yao imetimia! Na katika mechi ya kandanda……

**11.kundi**: Goaaaaaaal!!!! baoooooo!!!

**MSIMULIZI:** La, sivyo unavyofikiri…Roni hajafunga bao bali wao wamefungwa bao la pili. Kufikia mwisho wa mchuano huo

mabao yakawa ni 2:0 na Roni akaamini ndoto yake imefikia mwisho. Eveline kwa upande wake anafanya mkutano wla dharura na kamati yake ya kampeni.

**MUZIKI**

**<u>Onyesho la Nne: Mkutano wa Kamati</u>**

**SFX: Simu ambayo si ya Evelyn inalia**

**1.EVELINE:** Tafadhali zimeni simu zenu za rununu..Tuna tatizo kubwa la kujadili….

**SFX: Simu ya Evelyn inalia**

**2.EVELINE:** Samahani! Nimesahau kuizima simu yangu. Nitaijibu simu hii moja tu halafu nitarudi**…(anajibu simu)** Naam, ni nani? Unaweza kunipigia baadaye? Niko kwenye mkutano saa hii.

**SAUTI:** Ni jambo muhimu sana haliwezi kusubiri!!

**4.EVELINE**: Afadhali iwe hivyo kwani nimewaweka watu wakinubiri!!Wewe ni nani lakini? Namba yako siitambui.

**SAUTI:** Ni kwa sababu napiga kutoka kituo cha polisi.. Eveline unahitaji kuja hapa haraka unavyoweza babako amepigwa risasi akiwa kazini…

**6.EVELINE**( hofu) wapi? Oh! Hapana! Lini? Wapi?

**SAUTI**: Wewe njoo kituoni… nitakueleza kila kitu baadaye.

(aangua kilio) Je ame…ame….ame….

**SAUTI:** Wewe njoo tu…

**Mwisho wa Kipindi cha Saba:**

**MSIMULIZI:** Kisa kinaendelea.. Mapito amepigwa risasi. Nani aliyempiga risasi na kwa nini? Je inahusiana na Eveline. Je Eveline ataendelea na kampeni yake baada ya haya yote kutokea? Nini kitakachotokea kwa Betty na Roni baada ya mashindo yao makali? Jiunge nasi wiki ijayo upate kujua. Unaweza kukiskiliza tena kipindi hiki kwenye mtandao wa intaneti. Tovuti yetu ni www.dw_world.de/lbe. Hadi wiki ijayo, kwaheri.